HOTUBA YA JAJI MKUU MHE. PROF. IBRAHIM HAMIS JUMA KWENYE BARAZA KUU LA WAFANYAKAZI WA MAHAKAMA KATIKA UKUMBI WA PSSSF DODOMA TAREHE 16-17 MEI, 2024 JIJINI DODOMA

Wahe. Majaji wa Mahakama ya Rufani mliopo,

Mhe. Mustapher Siyani, Jaji Kiongozi,

Mhe. Dkt. Juliana Masabo, Jaji Mfawidhi Dodoma,

Wahe. Majaji Wafawidhi,

Wahe. Majaji wa Mahakama Kuu mliopo,

Mtendaji Mkuu wa Mahakama,

Makamishna wa Tume ya Utumishi wa Mahakama,

Mhe. Msajili Mkuu wa Mahakama,

Mhe. Naibu Katibu wa Tume ya Utumishi wa Mahakama,

Mhe. Kaimu Msajili wa Mahakama ya Rufani,

Mhe. Mtendaji wa Mahakama ya Rufani,

Mhe. Msajili wa Mahakama Kuu,

Watendaji wa Mahakama Kuu – Kanda na Divisheni,

Wahe. Naibu Wasajili,

Wakurugenzi na Watendaji wa Mahakama,

Katibu wa Baraza,

Wajumbe wote wa Baraza kwa nyadhifa,

Wageni waalikwa toka TUGHE Makao Makuu,

Ndugu wageni waalikwa,

Mabibi na Mabwana,

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA!

MAHAKAMA YA TANZANIA!

1. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, aliyetujalia uhai, afya njema na kutuwezesha kukutana hapa Dodoma siku ya leo. Aidha, nawashukuru viongozi wote wa mabaraza ya Kanda na Mikoa ya Wafanyakazi ambao wengi wenu mpo hapa leo, kwa kuweza kufanya vikao vya mabaraza hayo na hatimaye sasa kuleta hoja na mapendekezo yenu katika baraza hili kuu katika muhimili wetu.

2. Aidha nichukue nafasi hii kuwapongeza watumishi wote wa Mahakama kupitia kwenu wawakilishi wao, kwa kuendelea kuchapa kazi. Kila mfanyakazi wa Mahakama, ana umuhimu na uzito katika dhima ya utoaji wa huduma za

haki. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inapowaahidi watanzania haki ya kupata huduma za haki, mzigo wa kuhakikisha watanzania wanapata huduma hizo umebebwa na sisi wafanyakazi wa Mahakama.

3. Nawapongeza watumishi wote kwa kuendelea kutekeleza Mpango Mkakati wa Miaka Mitano awamu ya pili pamoja na programu ya Maboresho ya Miaka Mitano *(The Five-Year Judiciary Strategic Plan 2020/21—2024/25 and Citizen-Centric Judicial Modernisation and Justice Service Delivery Project)* ambazo zinalenga pia kutekeleza Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 *(Tanzania Development Vision 2025)*.

4. Ni vizuri kufahamu kuwa viongozi wa Mahakama wanatambua na kuheshimu sana mchango wa kila mtumishi wa Mahakama kwani kwa kuunganisha mchango wa mmoja mmoja ndiyo uliowezesha utekelezaji wa programu mbalimbali za kimaboresho.

5. Nina kila sababu ya kuwapongeza wafanyakazi wa Mahakama kutokana na kujituma kwenu kuhakikisha kuwa tunatekeleza kwa ufanisi mipango tuliyojiwekea. Tufahamu kuwa kupanga ni jambo moja na utekelezaji wa mipango ni jambo lingine, kwetu sisi tumepanga, tumetekeleza na tunaendelea kutekeleza.

6. Natoa rai kwa wafanyakazi wote kuwa daima tusirudi nyuma katika jitihada hizi za kimaboresho. Sote tushikamane katika kuhakikisha kuwa Mahakama inasonga mbele kwa kutoa huduma bora ya utoaji haki.

MATUMIZI YA TEHAMA YATATUWEZESHA KUTEKELEZA MIPANGO YETU KWA HARAKA NA UFANISI ZAIDI.

7. Katika hotuba yangu ya mwaka 2022 katika kikao cha Baraza la Wafanyakazi nilisema kuwa dunia imezidi kuwa kama Kijiji (tena huenda imefikia hatua ya kuwa kitongoji, na siku zijazo itakuwa kama mtaa tu). Kasi ya mabadiliko ya Teknolojia, inaongezeka kwa kasi kubwa sana na hakuna anayeweza kubashiri tutaishia wapi.

8. Nilisema pia kwamba Serikali imewekeza sana katika miundombinu ya TEHAMA katika taasisi zake.

9. Mradi wa Tanzania ya Kidijitali (*Tanzania Digital Project*) ulioanza mwaka 2021 ni kielelezo tosha kuwa Serikali imekusudia kwa dhati kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano na Mifumo ya Kidijitali kufanikisha shughuli za kiuchumi na kijamii.

10. Ni lazima Mhimili wa Mahakama tufaidike na uwekezaji mkubwa uliofanywa na Serikali yetu katika Mkongo wa Taifa wa Mawsiliano ambao ndio msingi wa Mahakama ya Tanzania kutumia mifumo ya kidijitali kutoa huduma za haki Tanzania. Kama ambavyo uwekezaji huu mkubwa umelenga kurahisisha na kufanikisha utoaji wa huduma za kiserikali kwa umma, uwekezaji huu wa Serikali katika Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano unawarahisishia wananchi upatikanaji wahuduma za Haki na za Kimahakama.

11. Nia ya uongozi wa Mahakama ni kuhakikisha kuwa, watumishi, ambao elimu na ujuzi wao haukuwatayarisha

kutoa huduma kwa njia za kidijitali, hawaachwi nyuma na mapinduzi makubwa ya kidijitali. Uongozi wa Mahakama una malengo makubwa ya kufanya kile kinachoitwa kwa lugha ya kiingereza—*Digital Upskilling*—kuwapa watumishi wote programu za mafunzo yanayolenga kuwajengea ujuzi na uwezo wa kutoa huduma katika mazingira ya kidijitali ili kuwaweka wafanyakazi sambamba na mapinduzi yatakayoletwa na Programu ya Tanzania ya Kidijiti. Mifumo ya TEHAMA inayotumiwa na Mahakama haitakuwa maana endapo watumishi wengi hawatakuwa na ujuzi na uwezo wa kutoa huduma za umma walizozoea kutoa kupitia makaratasi na majalada, hadi katika mazingira ya kidijiti. Katika jitihada za kuvuna faida zinazotokana na mradi wa Serikali uitwao TANZANIA YA KIDIJITALI, Mahakama ya Tanzania, kwa kushirikiana na Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto, iliandaa programu ya mafunzo maalum ya kuwapatia wafanyakazi ujuzi wa awali wa kidijitali (*Basic Digital Skills*). Nafahamu kuwa mafunzo haya yalishaanza na nimetaarifiwa kwamba mafunzo ya awali yalifanyika kuanzia mwezi Februari hadi Aprili 2024.

12. Aidha nimetaarifiwa kuwa hadi mwezi Aprili jumla ya watumishi **1785** walishiriki mafunzo hayo. Kati yao **1302** ni Wasaidizi wa Kumbukumbu na **483** ni Waandishi Waendesha Ofisi (Makatibu Mahsusi). Hili ni kundi muhimu sana linategemewa kuwa chachu kwa wengine kwa kuongoza katika matumizi ya TEHAMA.

13. Ni matumaini yangu na matarajio ya wadau wetu kuwa baada ya kupata mafunzo ya awali huduma zetu za kimahakama zitakuwa fanisi na zenye ubora zaidi. Mafunzo haya ya awali yawe kama madaraja ya kujiendeleza na kujiimarisha zaidi katika matumizi ya mifumo ya kidijitali. Kasi ya mabadiliko ya teknolojia za kisasa zinawataka watumishi wa Mahakama kuwa *"digital literate,"* kuwa na kasi ya kubadilika kadri teknolojia invyobadilika. Hakuna jambo la hatari kwa wafanyakazi pale mabadiliko ya kidijitali yatakapowaacha nyuma na kuwa *"digital illiterate."*

14. Ni vema wale mliotoa mafunzo muendelee kuwafuatilia wanafunzi wenu kwa lengo la kuhakikisha kuwa mafunzo mliyowapatia yanafanyiwa kazi na kama yameongeza tija au

la. Kwa maana nyingine ni lazima kufanya tathmini ya mafunzo kwa kulinganisha na huduma zinazotolewa na wafanyakazi wetu baada ya kupata mafunzo hayo.

MIFUMO MIPYA TEHAMA INALENGA KUBORESHA MAZINGIRA YA KAZI

15. Pamoja na ukweli kuwa mifumo ya TEHAMA inayotumiwa na Mahakama ya Tanzania inawalenga wananchi na watumiaji wa huduma za Mahakama kwa kuwapa huduma kwa weledi, ufanisi, uwazi na kwa haraka; sisi watumishi tupokee mifumo hii kwa kuwa inalenga kutuboreshea mazingira ya kuifanya kazi zetu za utoaji wa huduma.

16. Hivyo basi, tuupokee Mfumo Mpya wa Usimamizi wa Mashauri (e-CMS) kwa kutambua unaturahisishia kazi. Baadhi ya faida kubwa zitakazo rahisisha kazi zetu:

- Badala ya kupitia malundo ya majalada na karatasi kukusanya Takwimu, Mfumo huu utakusanya takwimu na taarifa mbalimbali kwa njia ya elektroniki, kwa usahihi. Takwimu zitatusaidia kuona yaliyojificha na kwa hivyo itatusaidia katika utekelezaji wa mipango mbalimbali na kuboresha jukumu letu la utoaji haki.

- Mfumo huu utasaidia kupima utendaji wa kila mmoja wetu bila ubaguzi au uonevu kwa watumishi. Utaongeza tija, ufanisi na uono wa viwango vya utoaji wa huduma wa kila mtumiaji wa mfumo huu, kwa mfano Majaji, Wasajili, Mahakimu, Masjala za Mahakama, wadau wote wa Mahakama.

- Watumishi watapunguza kukutana na wadaawa uso kwa uso na kuondoa lawama za kimaadili kwa vile wadaawa na wananchi watapata fursa ya kuingia katika mfumo kutafuta taarifa bila kumuona mtumishi wa Mahakama. Hakutakuwa na nafasi ya mtumishi kudhaniwa kuwa kapokea rushwa ili atoe huduma.

- Usimamizi wa wafanyakazi ni jambo muhimu sana katika utumishi. Mfumo huu utaboresha usimamizi na ukaguzi. Kwa mfano, Jaji/Hakimu Mfawidhi na Wasajili, wataweza kuona kila hatua ambayo shauri lolote linapitia na kufikia mbele ya Jaji au Hakimu, bila kuliita jalada au kuomba taarifa ya mashauri kutoka kwa aliye na jalada. Badala ya Wafanyakazi kupoteza

muda kutafuta majibu ya maswali yanayoulizwa na viongozi wao, viongozi watazipata hizo taarifa wakati wowote, wakiwa pahala popote katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

MFUMO WA TTS

17. Mfumo wa huu wa *Transcription and Translation Software (TTS)* umelenga kuwapunguzia watumishi (hususan) majaji na mahakimu, mzigo mzito wa kuandika mienendo ya mashauri kwa kalamu ya mkono. Mfumo huu unapokea sauti, uinakili hiyo sauti na kuiweka katika maandishi ya kiswahili, na unao uwezo wa kutafsiri hayo maandishi kutoka lugha ya kiswahili hadi kiingereza, na pia kutoka lugha ya kiingereza hadi kiswahili.

18. Mfumo wa TTS tayari umefungwa na kuanza kutumika katika mahakama 11, ikiwemo baadhi ya Mahakama Kuu (ambazo pia ni Masjala Ndogo za Mahakama ya Rufani). Nirudie kusisitiza kuwa, mfumo huu wa *TTS* utaongeza ufanisi katika uchukuaji wa mwenendo wa shauri kwa kumpunguzia Jaji/Hakimu mzigo wa kusikiliza na kuandika kwa wakati mmoja, na kuharakisha kupatikana kwa mienendo ya mashauri kwa ajili ya kukata rufani.

Kudijiti Nyaraka na Kumbukumbu za Mahakama

19. Wafanyakazi tunafahamu kuwa nyaraka za mashauri zina nafasi kubwa katika kuiwezesha Mahakama kutekeleza jukumu lake la msingi la utoaji haki. Mahakama ya Tanzania ni mzalishaji mkubwa wa kumbukumbu na nyaraka kupitia ngazi zote za mahakama. Aidha, wafanyakazi tunafahamu kuwa nyaraka na kumbukumbu za mahakama zisipotengewa maeneo ya hifadhi, huchukua nafasi chache zinazotumika na wafanyakazi kama ofisi zao. Mlundikano wa majalada ya zamani katika maofisi ya watumishi inaweza kusababisha maambukizo ya magonjwa na kuhatarisha afya ya wafanyakazi makazini.

20. Nawasihi wafanyakazi, tupokee mifumo ya miundombinu ya TEHAMA ambayo itatusaidia kuboresha uzalishaji, uchakataji, utunzaji na usambazaji wa nyaraka na kumbukumbu za Mahakama. Wafanyakazi tushiriki kikamilifu katika zoezi linaloendelea ya kuziweka nyaraka na kumbukumbu za Mahakama katika mfumo wa kidijiti.

TAARIFA YA MSAJILI MKUU YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA MAHAKAMA 2023

21. Taarifa ya Msajili Mkuu Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Mahakama ya Tanzania kwa mwaka 2023, inatoa picha muhimu ya namna watumishi wa Mahakama walivyotekeleza majukumu yao, sio tu kwa ufanisi na mafanikio makubwa, bali pia kwa namna walivyoweza kubainisha utekelezaji wa majukumu kisayansi kwa kutumia vigezo vya Mpango Mkakati wa Mahakama, vigezo vya Programu ya Maboresho, na kutumia pia takwimu zinavyotupima mmoja mmoja na pia kwa ujumla wa ngazi za Mahakama na kwa ujumla wa Mahakama ya Tanzania.

Mahakama ya Tanzania imefikia hatua ya kuweza kujieleza inafanya nini na kwa kiwango gani, mwaka hadi mwaka. Tunajitathmini na kujipima kwa vigezo vya—

- Mzigo wa mashauri aliyonayo kila Hakimu au Jaji au Msajili/ Naibu Msajili *(Caseload)*;
- Uwiano wa mashauri yaliyotolewa maamuzi dhidi ya mashauri yanayofunguliwa katika mwaka husika *(Clearance rate)*;

- Mashauri yanayoendelea zaidi ya muda uliokubaliwa kwa mashauri katika ngazi husika ya mahakama *(Backlog)*;
- Idadi ya mashauri ambayo Jaji wa Mahakama Kuu na Jaji wa Rufani inapandishwa katika TANZLII;
- Maamuzi ya mashauri yaliyokamilika na yanayosubiriwa kusomwa na muda kuzidi zaidi ya siku 90; na
- Utoaji wa nakala za hukumu mara baada ya kusomwa.

22. Nitumie Baraza hili kuwapongeza watumishi wote katika ngazi ya Mahakama za Mwanzo, kwa kuendelea kuwa "Mahakama ya Wananchi":

- Mahakama za Mwanzo ndizo zinazobeba mzigo mkubwa wa utoaji haki kwa wananchi wengi. Mahakama za Mwanzo zilibeba na zilisajili asilimia 71 ya mashauri yote katika mwaka 2023. Aidha zilisikiliza na kukamilisha asilimia 71 ya mashauri yaliyosikilizwa katika ngazi zote za Mahakama za Tanzania.

23. Natoa pongezi kwa wafanyakazi wote wa Mahakama kwa kuendelea kupunguza mlundikano wa mashauri mahakamani ili kuishi lengo letu la utoaji wa haki kwa wakati:

- Mwishoni mwa 2023, idadi ya mashauri ya mlundikano ilikuwa 2,594 sawa na asilimia 5 ya idadi ya mashauri 51,330 yaliyokuwa yakiendelea katika ngazi zote za mahakama. Kwa kulinganisha na mwaka 2022, iliyokuwa na mlundikano wa asilimia 6, mwaka 2023 mlundikano ulipungua kwa asilimia 1 (sio haba) ukizingatia kuwa usajili wa mashauri uliongezeka kwa asilimia 3 katika mwaka 2023 kutokana na mafanikio ya usajili wa mashauri kwa njia ya mtandao.

24. Msajili Mkuu ametumia kipimo cha “CLEARANCE RATE”— “Uwiano wa mashauri yaliyotolewa maamuzi dhidi ya mashauri yanayofunguliwa katika mwaka husika.” Lazima wafanyakazi mjipongeze, kwa kuamua kufikia **clearance rate** ya asilimia 100, ingawa malengo yetu yalikuwa mwaka 2023 kuamua asilimia 106.

HITIMISHO

25. Ndugu wajumbe wa baraza na wageni waalikwa, matarajio yangu ni kwamba, mwisho wa kikao hiki tutatoka na maazimio ya pamoja ambayo kwa upande wa Uongozi wa Mahakama nawaahidi kuwa yatakwenda kuyafanyia kazi kwa kiwango kinachostahili.

26. Kama nilivyoeleza hapo awali tutapokea taarifa mbalimbali kutoka menejimenti kuhusiana na masuala yaliyojitokeza katika baraza la wafanyakazi mwaka jana.

27. Naomba kuwasisitiza kusikiliza taarifa au majibu hayo kwa umakini ili mwisho tuweze kutoa michango kuhusiana na taarifa hizo na pia kuwapelekea wale tunaowawakilisha hapa katika baraza hili.

28. Nirudie tena kuwashukuru sana waratibu wa baraza hili kwa matayarisho na makaribisho mazuri hapa Dodoma. Kipekee niwashukuru viongozi wa Kanda ya Dodoma Mhe. Jaji Mfawidhi - Dodoma, Naibu Wasajili,

Mtendaji wa Mahakama wa Kanda ya Dodoma pamoja na Watumishi wote wa Kanda hii. Nasema kazi iendelee.

29. Ndugu wajumbe wa baraza na wageni waalikwa, napenda kuhitimisha hotuba yangu kwa kuwashukuru tena wafanyakazi wote wa Mahakama pamoja na Viongozi kwa kufanya kazi kwa bidii na ueledi mkubwa.

30. Niwahakikishie kuwa maazimio yote yatayofikiwa katika baraza hili yatatekelezwa na kupewa mrejesho mapema iwezekananvyo.

31. Baada ya kusema hayo, kwa furaha kubwa natamka rasmi kuwa Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa Mahakama ya Tanzania 2024, umefunguliwa rasmi.

ASANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA